# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI


***Simu***: **+255-26-2323189**
***Barua pepe***: **ps@moha.go.tz**
***Tovuti***: **www.moha.go.tz**
*Unapojibu tafadhali taja:*

**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**Mtaa wa Habari/Afya,**
**S. L. P 2916,**
**40483 DODOMA.**


**26 Aprili, 2024**

## TAARIFA KWA UMMA

**MSAMAHA WA MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWA WAFUNGWA KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 60 YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 26 APRILI, 2024**

Tarehe 26 Aprili, 2024 Taifa letu linaadhimisha Miaka 60 ya Muungano wa Tanzania. Hili ni tukio muhimu na la kihistoria kwa Taifa letu. Katika kuadhimisha sherehe hiyo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametumia mamlaka aliyopewa chini ya Ibara ya 45(1)(a) - (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa msamaha kwa wafungwa kwa masharti yafuatayo:-

1. (i) Wafungwa wote wenye sifa stahiki wapunguziwe robo ($\frac{1}{4}$) ya adhabu zao wanazozitumikia hivi sasa baada ya kutoa punguzo la kawaida la moja ya tatu ($^{1}/_{3}$) linalotolewa chini ya Kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Magereza Sura ya 58. Wafungwa hao sharti wawe wamehukumiwa kifungo cha kuanzia miaka miwili (2) na kuendelea ambao wametumikia robo $\frac{1}{4}$ ya adhabu zao gerezani na wawe wameingia gerezani kabla ya tarehe 28 Disemba, 2023, isipokuwa wafungwa walioorodheshwa katika sharti la 2(i – xi);

(ii) Wafungwa wagonjwa wenye magonjwa ya kudumu au sugu ambao wapo kwenye hatua ya mwisho "terminal stage". Ugonjwa na hatua hiyo vithibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa **Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya**;

(iii) Wafungwa wote wanaotumikia kifungo cha maisha gerezani ambao wametumikia adhabu zao kwa miaka kumi na tano (15) na kuendelea wabadilishiwe adhabu zao kuwa kifungo cha miaka thelathini (30);

(iv) Wafungwa wa kunyongwa waliomaliza taratibu za kimahakama ambao wamekaa gerezani kwa muda wa miaka kumi (10) na kuendelea wabadilishiwe adhabu ya kifo kuwa kifungo cha maisha;

(v) Wafungwa waliowahi kubadilishiwa adhabu kwa Msamaha wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka adhabu ya kifo kuwa kifungo cha maisha ambao wametimiza miaka kumi (10) na kuendelea tangu kupata msamaha huo, wabadilishiwe kifungo cha maisha kuwa kifungo cha miaka thelathini (30);

**(vi)** Wafungwa wazee wenye umri wa miaka sabini (70) au zaidi, umri huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa **Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya;**

(vii) Wafungwa wa kike walioingia na ujauzito gerezani au wenye watoto wanaonyonya au wasionyonya;

**(viii)** Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili wasio na uwezo wa kufanya kazi. Ulemavu huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa **Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya;**

(ix) Wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini (under presidential pleasure) ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka kumi (10) au zaidi.

2. Aidha, msamaha huo usiwahusishe wafungwa wafuatao:-

(i) Wafungwa wanaotumikia vifungo vya nje na wale waliowahi kukiuka masharti ya vifungo vya nje chini ya Sheria ya Bodi za Parole Sura ya 400 (R.E 2002), Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 (R.E 2002) na Kanuni za Kifungo cha Nje [The Prisons (Extra Mural Penal Employment) Regulations, 1968];

(ii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, rushwa na usafirishaji au kujihusisha kwa namna yoyote ile na madawa ya kulevya ikiwemo bangi;

(iii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya kujamiana, utekaji au wizi wa watoto, kupoka, kuwapa mimba wanafunzi au makosa yoyote yale yanayohusiana na ukatili dhidi ya watoto na kujihusisha kwa namna yoyote ile na biashara haramu ya binadamu;

(iv) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu, unyang'anyi, unyang'anyi wa kutumia nguvu, unyang'anyi wa kutumia silaha, kumiliki silaha, risasi, milipuko au kujaribu kutenda makosa hayo;

(v) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya kujihusisha kwa namna yoyote ile na nyara za Serikali au ujangili;

(vi) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani ambacho siyo cha maisha kwa makosa ya wizi au ubadhilifu wa fedha za Serikali;

(vii) Wafungwa wanaotumikia vifungo gerezani kwa makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo;

(viii) Wafungwa wenye makosa ya kujaribu kuua, kujaribu kujiua au kuua watoto wachanga, ugaidi, uharamia na makosa ya kimtandao (Attempt to Murder, Attempt Suicide, Infanticide, Terrorism, Piracy and Cyber crimes);

(ix) Wafungwa warudiaji na wale waliowahi kupata msamaha wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa kwa wafungwa walioainishwa katika sharti la 1(iii, iv na v);

(x) Wafungwa waliotenda makosa ya kinidhamu gerezani ambao makosa hayo hayajatimiza miaka mitatu (3) mpaka kufikia tarehe 26 Aprili, 2024;

(xi) Wafungwa wa madeni (civil prisoners).

3. Wafungwa elfu moja na themanini na mbili **(1,082)** wamenufaika na Msamaha huu ambapo wafungwa ishirini na tisa **(29)** kati yao wameachiliwa huru leo tarehe 26 Aprili, 2024, wafungwa ishirini (20) waliohukumiwa adhabu ya kifo wamebadilishiwa adhabu ya kifo kuwa kifungo cha maisha, wafungwa ishirini na saba (27) waliohukumiwa kifungo cha maisha wamebadilishiwa adhabu kuwa kifungo cha miaka thelathini (30) na wafungwa elfu moja na sita **(1,006)** wamepunguziwa adhabu zao na watabaki gerezani na kuendelea kutumikia sehemu ya kifungo kilichobaki. Ni matarajio ya Serikali kuwa wafungwa walioachiliwa huru leo tarehe 26 Aprili, 2024 watarejea tena katika jamii kushirikiana na wananchi wenzao katika ujenzi wa Taifa letu na kwamba watajiepusha kutenda makosa ili wasirejee tena gerezani.

**Daniel Baran Sillo**

**Kny: WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**